

KISWAHILI
MUHULA WA PILI 2024
KIDATO CHA KWANZA
MUDA: SAA 2:00
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

A. UFAHAMU

[1] ASIYESIKIA NA MKUU HUVUNJIIKA GUU

MKAIDI

UKAIDI WA MKAIDI

Sahihisha kichwa kingine chochote kinachoafiki kifungu hiki [1x1= 1]

[2] Kuitwa mama kabla ya kumkopo mwana wake mwenyewe [1x1= 1]

[3] -Alijiona kuwa ye ye ndiye mchukuzi bora
 - Aliwaona wenzake kama maua yaliyonyauka na lake ndilo kwanza linaonana na juu

[1x1= 1]

[4] -kwa kutosikiliza wakuu na kumkimbia mtu ambaye hata hakuwa anamuelewa vizuri

- pesa na raha alizokimbilia akawa anazisikia kama hadithi ndotoni [2x1= 2]

[5]- mumewe hakutulia mambo ya nje , alikuwa kiguu na njia

-Alikuwa na wanawake wengi nje ya ndoa (1x1=1)

[6] –kukonda

-homa hapa na pale

-vipelevipele mwilini [3x1=3]

[7] –walikuwa wakimfunza umuhimu wa kuwa na maadili [1x1=1]

[8] Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

Haraka haraka haina Baraka (1x1=1)

(9) [i] kosa makali

(ii) atafaulu

(iii)-akiwa bado mdogo /Bado hajakomaa

[v] vijinenoneno

(4x1=4)

B. MATUMIZI YA LUGHA

a) Ala tuli ni ala zisizosogea wakati wa kutamka kwa mfano meno, ufizi, kakaagumu, kaakaalaini, koromeo ilhali ala sogezi ni ala za kutamkia zinazosogea wakati wa matamshi kwa mfano midomo na ulimi. (2x1=2)

(b)

- i) /a/
- ii) /w/
- iii) /ch/
- iv) /e/

(1/2 ×4=2)

c). Silabi wazi ni silabi inayoisha kwa irabu mfano **ma-ma** ilhali silabi fungo huisha kwa konsonanti mfano i-l-ha-li, **m-tu** (2x1=2)

d) Tunga sentensi yenye kiunganishi cha masharti Nitakutunuku **iwapo** utawajibika. (1×1=1)

e) Wanafunzi **wasomao** kwa bidii watatuzwa (1×1=1)

f) amri; Kuja hapa!

rai/ombi; Tafadhalii njoo.
swali; Unataka nini?
Taarifa; Nitaenda sokoni.

Mshangao; Lo! Umemaliza chakula chote.

(3x1=1)

g) Mwimbaji alijinunulia **a'la** za muziki. (1x1=1)

h) Mwanamke yule **amenunua kitabu kizuri** (1×2=2/0)

i) **Mlalao**

Hakiki majibu ya mwanafunzi (1×1=1)

j)

M -wa :Mtu -watu
M -Mi :Mtume -Mitume
Ki -Vi :Kifaru -Vifaru
Ch -Vy :Chura -Vyura
Kapa -Ma :Daktari -Madaktari

(3x1=3)

k) Msipigane – **m;nafsi**
 si -; kikanushi
 an; kauli
 e; kiishio

(4x 1/2 =2)

l) mwalimu huyo/kitabu kikubwa; RN
huyo alikuwa/kikubwa mno; RV
jana jioni; RE
alikuwa akiandika; RT (3x1=3)

m)

1. Mnyama wa majini
 2. Kitendo cha kuketi
 3. Pande la kuni lililochomwa
 4. Kushinda mahali fulani
 atunge sentensi moja **(1×2=2)**


n)

S				
KN		KT		
N	V	T	N	V
Mkulima	hodari	hupata	mazao	tele

$(8 \times \frac{1}{2}=4)$

- o) 1. Uundaji wa nomino kutoka kitenzi - uimbaji, mwimbaji
 2. Mtendwa - amejipikia
 3. Ukubwa - jitoto, jitu

Atungie sentensi **MOJA**



(1×2=2)

- p) 1. Ufupishaji wa maneno/tarakimu - 'ndo badala ya ndio , '63-1963
 2. Kuonyesha sauti ya ving'ong'o - ng'ombe
 3. Kuonyesha silabi iliyotiliwa mkazo - ba'rabara

(2×1=2)

q) mdogo

- r) "Ala! Kwa nini hamjaelewa mada hii leo?" Mwalimu aauliza.
 Hakiki matumizi ya vihisishi vinginevyo

(1×3=3)

C. ISIMU-JAMII

a) Sajili ya hotelini; Kuna matumizi ya msamiati maalum wa hotelini kwa mfano menuy.

(kutaja, alama1, kuthibitsha, alama 1,jumla alama 2)

b)

- i. Matumizi ya lugha ya ucheshi na utani; moto kama pasi
- ii. Matumizi ya lugha legevu/isiyo sanifu; ugali kubwa
- iii. Matumizi ya msamiati maalumu; menuy
- iv. Lugha ya hotelini inaweza kuchanganya ndimi; mix
- v. Ni lugha shawishi na rahishi kuelewaka; mnakaribishwa, menuy hii hapa
- vi. Wakati mwingine kuna matumizi ya chuku; utapata yote baada ya sekunde.
- vii. Ni lugha ya kupumbaza na kufurahisha kwa kuwa inanuiwa kuvutia;mnakaribishwa
- viii. maswali na majibu;wapi toothpick? hizo hapo
- ix. sentensi fupi fupi; nimeshiba. Hizi hapa pesa.

$$(8 \times 1 = 8)$$

(Mwalimu atathmini majibu mengine ya wanafunzi, lazima mfano utolewe)

D. FASIHI SIMULIZI

a) i) Vitendawili ni semi zinazotolewa kwa mtu kama swalili afumbue

$$(1 \times 1 = 1)$$

ii)

1. Kitangulizi- Mtegaji: kitendawili

Mteguaji: tega

2. Swali lenyewe- kitendawili kutegwa

3. Majibu kutolewa

4. Mtegaji asipooridhika huomba kupewa zawadi kisha hutoa jibu.

$$(4 \times 1 = 4)$$

b)

- i. Vitendawili vina fomyula ilhali methali hazina fomyula
- ii. Fumbo la kitendawili hufumbuliwa papo hapo fumbo si lazima kufumbuliwa papo katika methali.
- iii. Vitendawili hutumiwa na watoto sana, methali hutumiwa kuonyesha hekima miongoni mwa watu wazima na wazee
- iv. Vitendawili hutolewa katika vikao maalum, methali si lazima kutengewa vikao maalum.
- v. Vitendawili hutumia lugha ya majibizano , methali aghalabu huwa kauli moja ya msemaji.
- vi. Hadhira tendi huwa katika vitendawili , katika methali hadhira si lazima iwe tendi.

(5x2=10)

